

TARGETER KCPE JARIBIO LA SITA STAHIKI

DARASA LA NANE - 2019

STAHIKI 006



KISWAHILI:

SEHEMU YA KWANZA:

Muda: Saa 1 Dakika 40.

LUGHA

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA
SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

NAMBARI YAKO YA MTHANI

JINA LAKO

JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mthani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mthaniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1-50, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano

Katika kijitabu cha maswali: Chagua jibu sahihi kutokana na maagizo uliyopewa

19. Chagua pambo lisilovaliwa katika kiwiko cha mkono.

A. Bangili.

B. Saa.

C. Usinga.

D. Kikuku.

Jibu sahihi ni C

Katika karatasi ya majibu

16. [A] [B] [C] [D]

17. [A] [B] [C] [D]

18. [A] [B] [C] [D]

19. [A] [B] [C] [D]

19. kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.

12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.



Huchapishwa na kuratibiwa na taasisi ya uchapishaji ya Targeter Educational Publishers Ltd.
Email: info@targeterpublishers.co.ke

GEUZA UKURASA

*Sana vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu
lifaalo zaidi kati ya yale iliyopewa.*

Lugha ya Kiswahili 1 tu hapa barani Afrika bali pia katika mabara 2. Ni jambo la ibra yaani
3 kusikia kuwa, Kiswahili hufunzwa nchini Marekani, Uchina na Ujerumani. Uamuzi huu 4 lugha
hii na hatufai tena 5. Mtu akijiifunza lugha hii ni vyema ajue kuwa baadhi ya sauti zake ni ghuna. Mfano
wa sauti ghuna ni 6. Dhima ya Kiswahili ni 7.

- | | | | | |
|----|-------------------------------------|--------------------------------------|------------------------------------|------------------------------------|
| 1. | A. inathaminiwa | B. inadhaminiwa | C. haithaminiwi | D. haidhaminiwi |
| 2. | A. nyingine | B. mengine | C. zingine | D. mingine |
| 3. | A. shani | B. kina | C. kuumua | D. jipya |
| 4. | A. umeidunisha | B. umeitwaza | C. umeitweza | D. umeikweza |
| 5. | A. kuitumia | B. kuizungumza | C. kuistahi | D. kuididimiza |
| 6. | A. m, f, g, h | B. v, z, du, ni | C. ch, s, d, t | D. n, gh, h, k |
| 7. | A. kututenganisha na kututambulisha | B. kututangamanisha na kutufanikisha | C. kututambulisha na kutuhamasisha | D. kutuunganisha na kututambulisha |

Nilikuwa na hamu ya kuwaona dada na kaka zangu yaani 8 wangu. Hivyo basi 9 kuelekea
mashambani. Nilipitia pale sokoni 10 11 ili kuwapelekea. Baada ya kuwasili walinipokea kwa moyo
mkunjufu. Nilitayarishiwa maakuli ya kufana 12 japo nilidinda na kuwaomba wanipakulie pure niliyozoca.
Walinicheka lakini mimi 13 nilijua faida ya pure. Waswahili husema 14. Niligundua kuwa asilimia
kubwa ya wapishi siku hizi 15 umuhimu wa vyakula vya kiasili.

- | | | | | |
|-----|------------------------------|-------------------------|----------------------------------|--|
| 8. | A. wanuna | B. masomo | C. maumbu | D. wavyele |
| 9. | A. nilishika tama | B. nilishika tariki | C. nilishika kani | D. nilishika hatamu |
| 10. | A. nilikonunua | B. nililonunua | C. niliponunua | D. nilimonunua |
| 11. | A. kikonyo cha zabibu | B. kikonyo cha nafaka | C. shule la zabibu | D. kishazi cha zabibu |
| 12. | A. sembuse | B. taraa | C. lau | D. japo |
| 13. | A. ndiye | B. ndie | C. ndimi | D. ndio |
| 14. | A. mgeni njoo mwenyeji apone | B. mgeni ni kuku mweupe | C. bura yangu sibatili na rehani | D. akomelepo mwenyeji na mgeni koma hapo |
| 15. | A. hawajui | B. hawapendi | C. hawasemi | D. haijui |

Kutoka swali la 16 mpaka 30. chagua jibu lililo sahihi.

16. Chagua jibu ambalo lina vihusishi pekee
A. halafu, tena, yake, zote
B. ili, bali, wala, kama
C. mbali na, baina ya, bila, ama
D. karibu na, kando ya, katika, kuliko
17. Ni sentensi ipi ambayo inetumia kwa ya kielezi.
A. Dereva alienda Ulaya kwa ndege.
B. Katika zoezi hilo nilipata alama sita kwa kumi.
C. Wenyeji wamewapokea wageni kwa moyo mkunjufu.
D. Mkimbizi alituzwa kwa kushinda mbio za mita elfu kumi.
18. Chagua sentensi yenye kiwakilishi kimilikishi
A. Msafiri wa nne alipata kibali lakini wale hawakupata.
B. Mfanyakazi wa tatu alistaafu lakini wengine walibakia.
C. Mtoto wao aliamka mapema lakini huyu alichelewa.
D. Mzazi wake alihudhuria sherhe lakini wangu hakuhudhuria.
19. Chagua sentensi yenye kiambishi -ki- cha vitendo kuendelea sawia.
A. Mwalimu alipoingia darasani wanafunzi walikuwa wakisoma.
B. Mama aliambua viazi huku akiimba.
C. Chandarua ki garini.
D. Ukisoma kwa bidii utafaulu mtihani wako.
20. Tambua na ya makubaliano
A. Nina kitabu cha hadithi.
B. Chakula kilipikwa na mjakazi.
C. Chaurembo na aongoze wimbo wa taifa.
D. Mgeni ana homa kali kwa sababu ya baridi.
21. Ni sentensi ipi ambayo ina "ci" ijeshi tamati
A. Kikulacho ki nguoni mwako
B. Shambani walipolima pana magumu mengi sana.
C. Mwanariadha aliyetuzwa medali ya dhidiata alifurahi sana.
D. Wanafunzi waliofuzu katika mtihani huo ndio watajiunga na kidato cha kwanza.
22. Tumia kiunganishi kifashe kujazia pengo. Mwanafunzi hataingia darasani _____ ya kubisha mlango.
A. mbali na
B. japo
C. madhali
D. minghairi ya
23. Sentensi, "Asingalikwenda kwake asubuhi, asingelikuta."
A. Hakuenda kwake asubuhi lakini alimkuta.
B. Alienda kwake asubuhi lakini hakumkuta.
C. Alienda kwake asubuhi na akamkuta.
D. Hakuenda kwake asubuhi wala hakumkuta.
24. Andika kwa wingi
Bibi anasukia ungo karibu na ua wako.
A. Mabibi wanasukia nyungo karibu na nyua zenu.
B. Bibi wanasukia maungo karibu na maua yenu.
C. Mabibi wanasukia nyungo karibu na maua yenu.
D. Bibi wanasukia nyungo karibu na nyua zenu.
25. Tofauti ya maana kati ya watano na wa tano ni
A. Watano ni idadi ya jumla na wa tano ni idadi kamili katika orodha.
B. Watano ni kuonyesha sifa na wa tano ni kuonyesha idadi.
C. Watano ni kuonyesha idadi kamili na wa tano ni anayechukua nafasi ya tano katika msururu.
D. Watano ni idadi kamili na wa tano ni idadi katika msururu.

26. Chagua sentensi inayofika mpyenyanjanishaji hizi
 (i) Kiata kilikuwa kidogo
 (ii) Kiata kilitoshia mgusi wake
 A. Law kiata kilikuwa kidogo kilitoshia mgusi wake.
 B. Kiata kilikuwa kidogo ngululahu kilitoshia mgusi wake.
 C. Licha ya kiata kuwa kidogo, kilitoshia mgusi wake.
 D. Maadamu kiata kilikuwa kidogo kilitoshia mgusi wake.

27. Tegua kitendawili kifuatacho
Kinasema hakionekani, kikikapitia huwezi kukishika.
 A. Usingizi.
 B. Upopo.
 C. Kisogo.
 D. Gari.

28. Cherono na Rahma ni mahibi zake Kesho Je, ndoa ya aina hii huitwaje?
 A. Mkenwenza.
 B. Mitara.
 C. Mwanyumba.
 D. Nasaba.



29. Chagua methali zote zinazotaka
 (i) Uaidharau ufa ufa janga ukata
 (ii) Vpata vyama vyu vi muji
 (iii) Samaki mkurija angaji mbachi
 (iv) Uaidharau kisereema chadima kadika jambo
 A. ii, iv
 B. i, ii
 C. i, iii
 D. iii, iv

30. Chagua jibu lenye jina la kike na kama kwa usahihi
 A. Witi - mwana.
 B. Maryaa - hankwa.
 C. Shangaizi - ami.
 D. Koo - pota.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.

Kwa kawaida hakuna mwanajamii ambaye hana dhima yake. Kigezo cha kugawa majukumu haya ni hali ya kimaumbile ya kuwa mwanamke au mwanamume. Umri pia huzingatiwa. Hii ndiyo sababu katika familia kuna majukumu ya baba, mama na hata watoto.

Dhima ya wanawake ilikuwa kukaa karibu na nyumbani, wakisaka matunda, majani na mizizi ambayo ingeletwa na wanaume. Baada ya nyama kufika, ilipokezwa mama. Mume alikaa kando. Majukumu yote ya jikoni alimwachia mwanamke. Mwanamke pia alifaa kulifanya pango mahali pema pa kuishi. Alitarajia kulipanga na kulitakasa ili lisitoe harufu *inayokirihisha*. Mwanamume naye alihakikisha kuwa kuna usalama wa kutosha kwa wote dhidi ya uvamizi kutoka nje au miongoni mwa wakazi walioishi pamoja nao au wanyama hatari. Wanawake pia walikuwa na jukumu la kuwatunza watoto jambo ambalo liliwafanya wasiende mbali na kwao.

Kwa upande wa vijana kazi yao kubwa ilikuwa kutema kuni na maji. Aidha ndio waliotumwatuwa hapa na pole. Walipoanza kuinukia, walifunzwa majukumu mengine ya watu wakubwa. Wavulana waliandamana na akina baba mawindoni na wasichana walibaki wakifanya majukumu ya mama zao. Ndio waliopanda, kupalilia na kuvuna mazao. Aidha walipeleka mazao sokoni na kubadilishana na kile walichokitaka. *Haya yakawa ngozi ya mwili ya jamii ambayo ilirithishwa vizazi baada ya vizazi.*

Ni kweli sasa tumepitia hatua mbalimbali za mabadiliko lakini kuna baadhi ya wanaajamii ambao wamekataa

katakata kubadilika. Kwao mgeu wa majukumu umesajia palepale pa enzi za mababu. Hawa ni wanamapokeo ambao huongozwa na taasubi za kiume inayowapendelea. Kwa wanamapokeo hawa, pindi msichana na mvulana wanapofunga nikahi kila mmoja ana majukumu yake. Ni dhima ya msichana kuhakikisha kuwa familia imepata lishe bora na kushughulika na usafi wa pale nyumbani. Yeye huhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni safi, watoto wanapata matibabu na uuguzi. Vilevile walihakikisha nidhamu ya watoto inaimarishwa na kudumishwa. Niliyokutajia hapa na majukumu ya kila mama awe amejiriwa au la. Tumewaona wengi walioajiriwa wakitaifuta huduma za vijakazi na lazima wakague iwapo majukumu yalitekelezwa ilivyostahili.

Naye mwanamume wa kisasa, ni jukumu lake kutafuta makazi, kuwa na hela za kuendesha shughuli za kifamilia na kukidhi mahitaji yote. Hata kama mwanamke anafanya kazi anayopokea mshahara, mwanaume ndiye huchukua majukumu nyeti yanayohitaji hela nyingi. Ni yeye atalipa malipo ya nyumba, kutoa fedha za matumizi ya safarini na kuweka mikataba ya kulipa fedha katika shirika la kifedha ili kufidiwa wakati wa majanga. Ni yeye pia huuchukua mkopo mkubwa wa kutekeleza jambo latakaloifaidi jamii. Na kama ilivyokuwa wakati wa zamani, kwa wanamapokeo ni muhali mwanaume kuingilia baadhi ya majukumu ya wanawake kama vile kupika na kufulia jamii nguo.

Wanamapokeo wajue kuwa kadri siku zinavyoendelea, watalazimika kubadilika bila hiari na kuacha udumishaji wa mgao wa majukumu kijinsia. Shinikizo zipo na ni nyingi kutoka kila jabibu. Watu wengi katika jamii wametambua kuwa ni upuuzi mtupu kuga wa majukumu kijinsia. Hayari tuko na ndoa za mzazi wa kipekee ambaye tumeona amejitwika majukumu ya kuendeleza familia na jamii bila kujali.

31. Chagua kauli isiyo ya kweli
- A. Kigezo kikuu cha kugawa majukumu huwa ni umri wa mtu.
 - B. Majukumu hugawa kulingana na jinsia ya mhusika.
 - C. Watoto hugawiwa kazi licha ya umri wao mdogo.
 - D. Uwindaji uliwanufaisha wanaume pekee.

32. Ni nini maana ya *inayokirihisha*
- A. inayodhuru.
 - B. inayoenea.
 - C. inayoibisha.
 - D. inayochukiza.

33. Kulingana na kifungu, majukumu ya kazi ya kijadi
- A. yalimfanya mwanamke aende mbali na alikoishi.
 - B. yalimfanya mwanaume kusalia nyumbani wakati wote.
 - C. yalimfanya mwanamke kuwa karibu na makao huku mwanamume akienda mbali nayo.
 - D. yaliwafanya wanaume na wanawake kusalia nyumbani wakati wote.

34. Haya yakawa ngozi ya mwili ya jamii ambayo ilirithishwa vizazi baada ya vizazi. Hii ina maana ya kuwa
- A. ilikuwa tabia ya wavulana kutema kuni na kuteka maji pekee.
 - B. ilikuwa mazoca kazi kugawanywa kulingana na mazoca.
 - C. kazi za wasichana zilipunguzwa huku zile za wavulana zikiongezeka.
 - D. ugoigoi wa vijana kazini ulionekana kwa kulemewa na majukumu yao.

35. Taasubi ya kiume
- A. inamtwisha mwanamke majukumu mengi kuliko mwanamume.
 - B. inamtwisha mwanamume majukumu mengi kuliko wanawake.
 - C. inawatwisha wanaume na wanawake majukumu sawa.
 - D. hawatwishi wanaume au wanawake majukumu zao.

36. vijakazi ni
A. anayefanya kazi ya kumwangelia mtoto pale nyumbani.
B. ni wanawake wanaofanya kazi za mabwana zao.
C. watumwa wanawake walioajiriwa kufanya kazi za nyumbani.
D. ni watumwa wanaume walioajiriwa kufanya kazi za nyumbani.
37. Mwanamke aliyeajiriwa,
A. hafai kufanya shughuli nyingine yoyote baada ya kutoka kazini.
B. ni juu yake kujua vile atavyokabiliana na majukumu yake ya pale nyumbani.
C. hutafutiwa na jamii husika mtu wa kumsaidia pale nyumbani.
D. huwatafuta vijakazi walioboea kazini ili wasisumbuke na ukaguzi wao wa kazi.
38. Aya ya mwisho inatuonyesha kuwa, kwa sasa
A. kazi zote zafaa kugawa kijinsia.
B. wanaume ndio wanafaa kuachiwa majukumu yote ya nyumbani.
C. wanawake ndio wanafaa kuachiwa majukumu yote ya nyumbani.
D. hakuna kazi za kike au za kiume.

39. Chagua kauli isiyo ya kweli
A. kazi kubwa ya wasichana wa kale ilikuwa kutema kuni na maji.
B. akina mama waliwaachia wasichana waliopevuka majukumu yao ya nyumbani.
C. lilikuwa jukumu la wanaume kuhakikisha kuwa usalama unaimarishwa pale bomani.
D. hata wa leo, kuna wale wangali wanatumia mfumo wa kijadi katika kugawa majukumu.

40. Ni yeye atalipa malipo ya nyumba, kutoa fedha za matumizi ya safarini na kuweka mikataba ya kulipa fedha katika shirika la kifedha ili kufidiwa wakati wa majanga.

Haya ni malipo gani mtawalia?

- A. Kodi, ada na karisaji.
B. Kodi, masurufu, ridhaa.
C. Pango, masurufu, bima.
D. Marupurupu, kodi, riba.

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.

Naam, siku niliyoisubiri kwa hamu na hamumu iliwadia. Niliwasili katika shule ya upili ya Ghara. Nilipofika, nilikuwa nimeandamana na baba yangu. Baada ya shughuli za hapa na pale, nilijuana na Bi. Safi. Yeye ndiye angenifunza somo la Kiswahili. Alikuwa mwalimu mlezi wa darasa langu. Kumbuka Bi. Safi ndiye aliyekuwa **akiwasajili** wanafunzi wa kidato cha kwanza. Mara aliponiona nikitembea kwa woga ubavuni pa baba yangu, aliondoka na kutoka kitini pake na kutukaribisha. Uso wake ulinikumbusha marehemu mama yangu ambaye pia alikuwa mwalimu wa shule za msingi. Bi Safi alivikagua vyeti vyangu na kuhakikisha kuwa havikuwa vimebatilishwa. Baada ya yote aliandika jina langu katika orodha ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na kunihakikishia kuwa yeye ndiye angekuwa mlezi wangu.

Darasani masomo yalikuwa mawe.

Tamrini za darasani zilimhitaji mtu kutumia ujuzi wake kuzijibu badala ya kukariri mawazo jinsi nilivyokuwa nimezoea. Ugumu wa masomo ulizidishwa na ugeni wangu shuleni. Shule hii ilikuwa miongoni mwa shule chache za kisasa zilizojengwa kwa kufuata ustaarabu wa kisasa. Ilinibidi nijizoeshe kutumia vifaa vya kisasa kama vile

vya vya kufyatua na kubonyeza swichi ili mlango ufunguke. Haya yote yaliniwia vigumu mno. Kwa kuwa mficha uke hazai ilimibidi kila mara kumwendea Bi. Safi ili anionyeshe. Ndiye kila mara alinitia shime nisiende nguu.

Naam, maisha ni hatua na wakati una mabawa. Ugeni uliisha na nikaanza kuingiliana na wenyeji. Wakanifunza njia za mkato za kufanya mazoezi hapo darasani. Niliona kila mmoja alijaribu kunizaini kwa yake ya upekee. Mimi nami nikawa bendera ambayo daima hufuata upepo.

Bi. Safi naye alitambua kwa kasi ya umeme mabadiliko katika kitiba changu. Sikuwa tena yule mwanafunzi aliyepokelewa siku ya kwanza shuleni. Alinijua kama mwanafunzi mwenye haja na mara nyingi nilijibu maswali darasani huku nikitetemeka. Nilikuwa nimekomaa sasa kiumri na kimatendo ila mawazo yangu yalikuwa yaleyale.

Waswahili husema tahadhari kabla ya hatari. Aidha usipoziba ufa utajenga ukuta. Bi. Safi aliniita ofisini mwake na kusema, "Tangu nikutane nawe ulipojiunga na shule hii nimeona mabadiliko makubwa katika tabia yake. Ulikuwa mwanafunzi mwenye bidii za mchwa ajengaye kichuguu kwa mate. Ingawa mlikuwa na matatizo mwanzoni, uliweza kumenyana nayo bila tabu. Lakini kwa sasa kuna jambo linaloisumbua nafsi yangu. Tangu uingine katika kidato cha tatu, masahibu zako wengi wamekuwa wanafunzi ambao wana tabia za unobe. Baadhi yao wameonyeshwa lango la shule kwa visa vya utovu wa nidhamu. Wiki iliyopita mwalimu wa zamu alikupata ukipiga kelele darasani licha ya kutofanya ziada na majoezi mengine darasani. ***Kwani unaharibika unapokaribia kuhitimisha masomo yako?***"

Nilimtupia jicho Bi. Safi kwa muda. Tayari nilikuwa nimemea pembe moyoni na nilishindwa ni kwa nini alijihushisha na maisha yangu. Hapo nilijiwa na kumbukumbu za mauko ya mama yangu, ujane wa baba yangu wa mwongo mmoja na jinsi alivyokazana kuhakikisha kuwa tulipata mahitaji yote ya kimsingi. Baba yangu daima alishinda kuniambia kuwa elimu ni ufunguo wa maisha.

Bi. Safi naye alikuwa amekata kauli kukiwahi chuma kili moto. Alinishauri kujiepusha na makundi ambayo yangeishia kutumbukiza jina langu mashuzi. Alinisihi kuvazingatia masomo yangu zaidi na kutumia muda wangu vizuri ili nisizame kimasomo. Kumbuka Bi. Safi alikuwa tayari amenitafutia udhamini na sikuwa nikilipa karo kuanzia kidato cha pili.

Baada ya kujisuta moyoni niliamua kuwa na mwamko mpya. Nilitanabahi kuwa nilikuwa na mwaka mmoja tu wa kuandaa mustakabali wangu. Kuanzia hapo nikaamua kuwa dereva wa kudhibiti maisha yangu.

41. Siku ambayo msimulizi aliisubiri kwa hamu na hamumu ni
- A. ile angekutana na Bi. Safi ambaye angekuwa mwelekezi wake shuleni.
- B. ile ambayo angeingia mjini Ghara kupambana na hali yake ya maisha.
- C. ile ambayo angeanza masomo ya shule ya upili.
- D. ile ambayo angeandamana na baba yake katika safari ya kuelekea chuleni.

42. Kulingana na kifungu, neno 'akiwasajili' lina maana gani?
- A. Akiwapokea.
- B. Akiwakaribisha.
- C. Akiwakagua.
- D. Akiwaandikisha.

43. Kulingana na aya ya kwanza
A. baba yake msimulizi hakuweza kuitambua hofu ya mwanawe.
B. Bi. Safi alishuku kwamba vyeti vya msimulizi vilibatilishwa.
C. baba yake msimulizi alikuwa rafiki yake Bi. Safi.
D. msimulizi aliyaogopa mazingira yake mapya.
44. Unadhani ni kitu gani kilichomfanya msimulizi kumkumbuka marehemu mama yake?
A. Kulingana na jinsi Bi. Safi alivyotabasamu.
B. Kutokana na ukweli kuwa mama yake msimulizi alikuwa mwalimu kama Bi. Safi.
C. Kutokana na kusimama kwa Bi. Safi kwenda kumkaribisha baba yake.
D. Ukweli ni kwamba Bi. Safi alifanana sana na mama yake msimulizi.
45. Kulingana na aya ya tatu
A. msimulizi alikuwa na msimamo thabiti.
B. msimulizi aliwafunza wenyeji njia za mkato za kufanya ziada.
C. msimulizi alikuwa hana msimamo.
D. marafiki zake msimulizi walimfanya afukuzwe shuleni kutokana na vitiba vibaya.
46. Ni kauli gani isiyo ya kweli kulingana na kifungu ulichokisoma.
A. Msimulizi alizoca kuyakariri mawazo yake alipokuwa katika shule ya msingi.
B. Changamoto huongezeka pale mtu asipozoeana na mazingira.
C. Ugumu wa masomo ulimfanya msimulizi kuchukia masomo.
D. Msimulizi hakuwa na ujuzi wa kutosha uliohitajika kujibu maswali katika shule ya sekondari.
47. Bi. Safi alikuwa na uwajibikaji kwa kuwa
A. alimwita msimulizi kujadili shida yake baada ya kuona mabadiliko katika tabia zake.
B. baada ya kuona woga wa msimulizi, aliamua kwenda kumlaki.
C. aligundua kuwa msimulizi aliwahi kushikana na mwalimu wa zamu akipiga kelele darasani.
D. aliamua kuwa mlezi wa msimulizi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.
48. Ni wazi kwamba
A. shule ya upili ilikuwa shida tupu kwa msimulizi.
B. msimulizi alifika katika shule ya upili ya Ghara na kuanza kupotoka mara moja.
C. Mwadishi alijifunza mambo mengi mazuri na mengine mabaya.
D. wanafunzi wote katika shule ya Ghara walikuwa watundu.
49. Kwani unaharibika unapokaribia kuhitimisha masomo yako? Je, ni methali gani inayowiana na kauli hii?
A. Kenda i karibu na kumi.
B. Elimu ni taa gizani huzagaa.
C. Baada ya kisa mkasa.
D. Mumunye huharibikia gizani.
50. Maana ya, "*Wameonyeshwa lango la shuleni*" ni
A. Wameyaasi masomo yao.
B. wamefukuzwa kutoka shuleni.
C. wamehimizwa kubadili mienendo.
D. mienendo yao imeanza kutiliwa shaka.